MTANDAO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU (THRDC)

# TAMKO JUU YA HALI YA WANAHABARI NA UHURU WA HABARI TANZANIA

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu awali ya yote unapenda kupongeza juhudi za Mhe. Rais John Pombe Magufuli za kupambana na rushwa na matumizi holela ya mali zaumma katika siku zake 100 toka aingie madarakani. Pamoja na pongezi hizi, Mtandao umebaini kuwa katika siku hizi 100 kuna mambo mengi yahusuyo haki za binadamu, uhuru wa habari ,demokrasia na utawala bora ambayo hayakwenda vizuri katika siku hizi za awali za serikali mpya ikiwemo suala la Zanzibar. Tamko letu hili limejikita zaidi katika kuangalia hali ya usalama wa wanahabari na uhuru wa kupata habari katika siku 100 za Serikali mpya.

Mtandao umekuwa ukifuatilia hali ya usalama wa wanahabari, uhuru wa habari na haki ya kupata taarifa katika mchakato wa uchaguzi yaani kabla ya uchaguzi mkuu na baada ya uchaguzi mkuu. Wakati wa uchaguzi mtandao wa watetezi wa haki za binadamu ulibainisha kuwa wanahabari katika baadhi ya maeneo nchini wanafanya kazi katika mazingira hatarishi ambapo wengine wao wamepokea vitisho na wakati mwingine kunyanyaswa, mfano chombo cha habiri Kyela Fm Radio ya Jamii ilifungwa kwa sababu za kisiasa.

Hatahivyo, hali ya usalama wa wanahabari kwa kipindi cha uchaguzi mwaka 2015 haikuwa ya kushtua ukilinganisha na miaka mingine ya uchaguzi iliyopita na hili linaweza kuwa ni tokeo la maandalizi ya usalama kwa wanahabari yaliyofanywa kwa wakati husika kati ya Mtandao na wadau wengne kama vile Baraza la Habari na kamati maalumu iliyoundwa chini ya UNESCO.

Mtandao wa Watatezi wa Haki za Binadamu umeshangazwa na na hali mpya inayojitokeza ya uvunjifu wa uhuru wa vyombo vya habari na haki ya kupata taarifa hasa katika kipindi hiki cha siku 100 za utawala mpya wa Taifa hili. Katika kipindi cha mwanzo cha serikali mpya mtandao umeshaweka bayana matukio kadhaa ya wanahabari kunyanyaswa na kupokea vitisho, kunyimwa kufanya kazi zao nahata kufutwa kwa gazeti la habari za kichunguzi la Mawio.

Kwa mfano, Sheria ya Gazeti ya mwaka 1976 imendelea kutumika kuvunja na kukiuka Uhuru wa habari na kupata taarifa nchini Tanzania. Kama ilivyotokea kwa gazeti la **Mwanahalisi** mnamo mwezi wa Saba tarehe 30 mwaka 2012 na kusitishwa kwa muda mfupi kwa gazeti la **Mwananchi** na **Mtanzania** iliyotokea mwaka 2013. Serikali ya sasa imefungia moja kwa moja machapisho ya Kiswahili ya gazeti linalotoka kila wiki la **'Mawio'** kwa Tangazo la Serikali (GN) namba 55 iliyotolewa tarehe 15 mwezi wa kwanza mwaka 2016. Tumestushwa na hali hii kwani serikali yoyote yenye lengo la kuwasaidia wanachanchi au yenye lengo la kupambana na rushwa ni lazima suala la uhuru wa habari, uwazi na ukweli liwe kipaumbele chake.

Mtandao umezungumza na msajili wa Magazeti na mwanasheria wa Wizara ya Habari, Tamaduni na Michezo na kupata taarifa kwamba, wizara husika imefungia gazeti la Mawio kutokana na taarifa iliyobebwa katika gazeti hiyo iliyokuwa na kichwa cha habari ''**Machafuko**

**yaja Zanzibar''**. Kutokana na serikali, hii taarifa ilikuwa ni ya uchochezi na ilikuwa ina viashiria vyote vya kuvuruga Amani ya nchi.

Msajili wa magazeti nchini alisema kuwa adhabu hiyo iliyotolewa kwa gazeti `la Mawio ilikuja baada ya uongozi wa gazeti hilo yaani wahariri kupewa tahadhari juu ya namna na aina ya uandishi wa taarifa zao ikiwemo na vikao mara kumi na sita (16) bila ya mafanikio. Msajili aliongeza kuwa, uongozi wa gazeti la Mawio umeshindwa kusimamia misingi ya taaluma ya uandishi wa habari.

Tumegundua pia, Waziri husika hakutumia vipengele vya Sheria ya Magazeti tu bali aliendа mbali na kufungia usambazaji wa gazeti hilo kwa namna yoyote ile ya ki elektroniki kama vile matumizi ya mtandao na haya kwa posta kupitia Sheria ya Posta (EPOCA). Hatua hii imeamsha shauku ya wadau wengi ikiwemo wanasheria, na wanataaluma mbalimbali wakilaumu kitendo cha waziri mmoja kutekeleza sheria asiyokuwa na mamlaka nayo bali mwenye mamlaka ni Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mtandao ulipata nafasi ya kuuliza juu ya mkanganyo huu na mwanasheria wa wizara ya Habari, Tamaduni na Michezo alielezea kuwa chini ya kifungu cha tatu (3) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) inatafsiri Waziri husika kuwa Waziri anayehusika na Mawasiliano tofauti na yale yanayolenga maudhui na usambazaji wa taarifa kwa huduma za kielektroniki kama za redio na televisheni; hii inamaanisha kuwa kwenye maswala ya maudhui waziri wa Habari, Tamaduni na Michezo ndiye anayehusika.

Hata hivyo, Mtandao ulifanya utafiti juu ya sheria tajwa na kutambua kuwa mbali na Waziri wa Habari, tamaduni na michezo kuwa na mamlaka ya kusimamia maswala ya maudhui chini ya sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010, sheria haimpi mamlaka ya kusimamisha uchapishaji na usambazaji wa gazeti . Kipengele cha 114 cha sheria hii kinatoa mamlaka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania yani TCRA na si kwa Waziri, hivo baadhi Waziri wa Habari alijipa madaraka asiyokuwa nayo kisheria .

Serikali ilikubali kuwa gazeti la Mawio lilifungiwa kabla uongozi wa hazeti hilo haujajibu barua yao ya mwisho ya mashtaka iliyopewa na wizara ili kutoa majibu. Mtandao ulitafsiri hatua hii kama **kukiukwa kwa haki ya kusikilizwa ambayo ni haki ya Kikatiba.** Utaratibu wa aina hii ulitumiwa pia katika kusitishwa kwa gazeti la Mwanahalisi mnamo mwaka 2012 na ulipingwa na Mahakama Kuu katika maamuzi yalifofikiwa mwaka 2015 ambapo Mahakama Kuu ilisema gazeti la Mwanahalisi lirudishwe katika utendaji kazi wake kwani wakati wa kulifungia serikali haikuzingatia taratibu na haki ya kusikilizwa.

Kwa miaka kadhaa sasa Sheria ya Magazeti imekuwa ikiorodheshwa kama sheria inayokiuka uhuru wa kujielezea, sheria hii imempa waziri mwenye dhamana nguvu kubwa mno. Sheria ilirithiwa kutoka katika uongozi wa Mkoloni na hiyo ilitengenezwa kwa kusudi la kukandamiza sauti ya watawaliwa. Hivyo kuna umuhimu wa serikali kuchukua hatua haraka iwezekanavyo.

Kwa kuzingatia sheria na vigezo vya kimataifa, ufungwaji wa gazeti la mawio umekiuka kipengele cha **19 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR)** na Mkataba wa Kimataifa wa Afrika ambao Tanzania imeridhia. Pia serikali imekiuka kipengele **cha 18 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambayo inatoa uhuru wa kujieleza

na wa kutoa maoni. Ni muhimu kutambua kuwa kufungiwa kwa gazeti la mawio kumevunja haki ya kupata taarifa kwa umma.

Mtandao unapinga vikali kitendo cha polisi kuwaita wahariri wawili wa hazeti la mawio na kutaka kuwatuhumu kwa kufitini nchi. Siku ya jumatatu juma lililopita wahariri wa Mawio wajulikanao kwa majina ya **Jabir Idrissa** na **Simon Mkina** walihojiwa na polisi juu uandishi wa gazeti katika maswala ya Zanzibar, kulingana na Maelezo ya Jabir mmoja wa wahariri hao alisema waliachiwa kwa dhamana siku inayofuatia baada ya Jukwaa la Wahariri nchini kusisitiza waachiliwe. Wahariri hao waliamriwa kurepoti kila siku katika kituo cha polisi mpaka pale watakapo pewa taarifa ya kuacha kufanya hivyo. Hakuna mashitaka maalum yaliyo wasilishwa juu yao.

Katika hatua nyingine siku 100 za Serikali mpya zimedhihirisha kuwa utawala huu hauheshimu baadhi ya misingi ya haki za binadamu na utawala bora hasa pale Wizara ya Habari ilipopeleka hoja Bungeni ya kufuta vipindi vya moja kwa moja (Live) toka vikao vya Bunge. Kwa miaka 10 katika serikali ya awamu ya nne wananchi wamekuwa wakiwafuatilia moja kwa moja wawakilishi wao bungeni na kuweza kujua mambo mengi yahusiyo mustakabali wa Taifa. Kitendo cha kuzuia matangazo ya moja kwa moja ya Bunge ni kuvunja Ibara ya 18 (2) ya Katiba ya Tanzania inayosema "*Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii"*

Kwa ujumla hali hii imefanya wanahabari na vyombo vya habari hapa nchini kuwa hofu kubwa katika kipindi hiki. Vyombo vya habari kufanya kazi kwa hofu kubwa kutaadhiri kwa kiwango kikubwa uhuru wao na upatikani wa habari za kichunguzi kwa maslahi ya Taifa. Mtandao umebain hali ya utoaji wa taarifa za kina zenye maslahi kwa umma unazidi kupungua kutoka na hofu inayojengekeka miongoni mwa wanahabari.

Serikali yoyote ili iweze kupambana na rushwa ni lazima itoe uhuru wa kutosha kwa vyombo vya habari na hasa wanahabari wa taarifa za kiuchunguzi ili kuisadia kuibua maswala ya rushwa. Taarifa nyingi za rushwa katika serikali ya awamu ya nne kama vile Richmond and Escrow zilitokana na taarifa za kiuchunguzi za vyombo vya habari. Hivyo tungetegemea serikali hii ya Mhe Magufuli ingekuwa mstari wa mbele kutumia vyombo vya habari katika vita dhidi ya rushwa badala ya kuvitia hofu katika utendaji wao.

**Mtandao wa Watetezi wa Haki Za Binadamu Unatoa Wito Juu ya Mambo Yafuatayo:**

i. **Kwa serikali**

- Serikali ifungulie gazeti la Mawio na kuipa adhabu nyingine ndogo ukizingatia kuwa kitendo cha kulifuta kabisa gazeti si cha kidemokrasia na doa Serikali ya Rais Mangufuli inayoonekana kuwa mstari wa mbele kupambana na rushwa hapa nchini.
- Huu ni wakati muafaka kwa Sheria ya Vyombo vya Habari na Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa kutengenezwa kwa muundo ambao unazingatia mapendekezo ya wadau ili nchi iweze kuwa na sheria zinazozingatia viwango vya kimataifa.

- Tunaisihi Serikali ibadilishe wazo lake kuzuia matangazo ya moja kwa moja ya Bunge ili kuwapa fursa wanachi kujua wawakilishi wao wanafanya nini bungeni na pia wananchi kuweza kufuatilia mambo ya msingi yahusuyo Taifa hili.
- Kwakuwa Rais Magufuli ameelekeza nguvu nyingi kwenye kupambana na rushwa tunamshauri aweke mazingira mazuri kwa vyombo vya habari katika utawala wake ili viweze kumsaidia kujenga Taifa lisilokumbatia rushwa na linaloheshimu misingi ya utawala bora.

**ii. Kwa Vyombo vya Habari**

- Vyombo vya habari nchini viungane kwa pamoja na kuachilia mbali tofauti zao ili viweze kuyazungumzia maswala haya kwa umoja na kuweza kujisimamia katika misingi yake ya kutoa taarifa.

- Watendaji katika vyombo vya habari haswa wanahabari na wahariri kuzingatia maslahi na Usalama wa Taifa na pia kusimamia misingi ya Taaluma ya Uandishi wa Habari.

- Kuungana pamoja na Mtandao wa Wateteiz katika kufatuna namna ya kuipinga Sheria ya Magazeti katika vyombo vya haki vya ndani na vya nje. Mtandao unaangalia uwezekano wa kisheria wa kupinga Sheria ya Magazeti hasa vifungu vinavyompa Waziri nguvu kubwa ya kuwa mlalamikaji, muendesha mashtaka, mpelelezi na mtoa maamuzi kwa wakati mmoja bila hata ya kumsikiliza mlalamikiwa.

**iii. Kwa Jumuiya ya Kimataifa**

Tunavisihi vyombo vya Kimataifa hapa nchini na Wadau wa Maendeleo wenye ushirikiano mzuri na serikali ya Tanzania, kwa kuzingatia protokali za kidiplomasia kuendelea kuishauri Serikali Tanzania kuheshimu misingi ya utawala bora, haki za binadamu hasa hasa uhuru wa maoni na haki ya kupata taarifa ambayo ndio msingi bora wa kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uendesha wa Taifa lao.

Imetolewa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu

**Onesmo Olengurumwa**

**Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC)**